BARAZA LA TAIFA LA ELIMU YA UFUNDI NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI (NACTVET)

# TAARIFA KWA UMMA

## MATOKEO YA UCHAGUZI WA UDAHILI KUPITIA MFUMO WA UDAHILI WA PAMOJA (CAS) KWA KOZI ZA AFYA NA SAYANSI SHIRIKISHI KWA MWAKA WA MASOMO 2026/2027 - AWAMU YA KWANZA

Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET) linautaarifu umma kuwa matokeo ya uchaguzi wa awamu ya kwanza kwa waombaji wa programu za Afya na Sayansi Shirikishi kwa mwaka wa masomo 2026/2027 yanatangazwa rasmi leo tarehe 31 Julai, 2026.

Jumla ya waombaji **26,705** walikamilisha maombi ya udahili; kati ya hao, waombaji **17,979** wamechaguliwa kujiunga na vyuo vinavyotoa programu za Afya na Sayansi Shirikishi, ambapo wanawake ni 8,936 (49.7%) na wanaume 9,043 (50.3%). Aidha, waombaji 5,572 (31.0%) wamechaguliwa katika vyuo vya Serikali, na waombaji 12,407 (69.0%) wamechaguliwa katika vyuo visivyo vya Serikali.

Aidha, waombaji wenye sifa ambao hawakuchaguliwa kutokana na ushindani katika programu na vyuo walivyoomba, wanashauriwa kuomba kujiunga na programu zingine katika vyuo vyenye nafasi katika dirisha la awamu ya pili kupitia Mfumo wa Udahili wa Pamoja.

Waombaji wote wanaweza kuangalia matokeo ya uchaguzi kupitia tovuti ya Baraza (**www.nactvet.go.tz**) kwa kubonyeza **CAS Selection 2026** kwa ajili ya kupata taarifa zaidi.

Baraza linautaarifu umma kuwa dirisha la awamu ya pili limefunguliwa rasmi tarehe 31 Julai hadi 21 Agosti, 2026 na matokeo ya uchaguzi yatatolewa tarehe 04 Septemba,2026.

Aidha, wale wanaohitaji kubadilisha programu au chuo, dirisha la uhamisho litakuwa wazi kuanzia tarehe 10 hadi 21 Agosti, 2026, hivyo watumie dirisha hili kukamilisha maombi hayo kupitia tovuti ya Baraza kwa kutumia akaunti yake aliyotumia kutuma maombi wakati wa awamu ya kwanza.

**Imetolewa na:**
**Kitengo cha Mawasiliano na Masoko**
**NACTVET**
**31/07/2026**

NACTVET Makao Makuu, Jengo la Kambarage - Ghorofa ya 7
S. L. P 387, Dodoma | +255 736 310311 | info@nactvet.go.tz | www.nactvet.go.tz